# KUNA KUINUKA TENA (WIMBO WATULIZENI MOYO NA AMANI KWAYA).
# MAANDIKO: AYUB. 19:25-27, 22:29.

## 1. UTANGULIZI

**Ufahamu** huu mkubwa aliokuwa nao Ayubu wakati anapitia katika majaribu mbali mbali na mazito na yanayouma kwa lengo la kutaka kumvunja moyo kabisa na yeye Ayubu akazidi kumpenda Mungu zaidi hata kuliko wakati alipokuwa hana majaribu ni siri kubwa aliyopewa na Roho Mtakatifu mwenyewe.

- Kitendo cha kuwa na ufahamu huu kwamba, pamoja na mwili wangu huu kuharibiwa na adui namna hii, iko siku moja nitatoka kama Dhahabu. ***Ayub 23:10.*** **Hii ni neema ya ajabu sana kama Yesu alivyokuwa nayo.** ***Math. 16:21-23, 27:63.***
- Lengo la adui la kutushambulia katika maeneo mbali mbali ya maisha haya ni kutaka tuvunjike moyo na kisha tukate tamaa kabisa na ikibidi tumwache Yesu!! **Na ndilo lilikuwa lengo lake kubwa kwa Ayubu tangu mwanzo wa majaribu yake.** ***Ayub. 1:9-11, Ayub 2:4-5.***
- Lakini Ayubu alimduwaza (alimwacha shetani midomo wazi) kwa kuwa alikuwa na ufahamu huu ndani yake wa kujua kwamba **" KUNA KUINUKA TENA BAADA YA ADUI KUANGUSHA CHINI KILA AINA YA MAFANIKIO NA BARAKA ALIZOKUWA NAZO!!** ***Ayub 22:29.*** **Kila mteule akipewa ufahamu huu na Roho Mtakatifu akawa na uhakika moyoni mwake kwamba kuna kuinuka tena; hakuna jaribu litakalomyumbisha kabisa.**

2. Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, alipenda sana kuwaendea wale ambao walikuwa wamekata tamaa sababu ya Mapito magumu waliyokuwa wanapitia na kuwatuliza mioyo yao na kisha kuwainua wale wote waliokuwa wamaekata tamaa. ***Luk 8:49-56*** **(Kijana inuka) (Maid/ Child Arise**) Na baada ya Kijana huyu kuinuka; wazazi wake walistaajabu sana!! Imani zao ziliinuka kwa upya na wakampenda Bwana Yesu kuliko awali. (**Yesu amekuja ili wenye viburi wote waanguke, bali walio wake wainuke tena.** ***Luk 2:34.***

- Mitume Petro naye kwa **Style** kama hii Bwana Yesu maana alikuwepo siku Kijana huyu anaambiwa na Bwana Yesu kwamba

kijana **INUKA**, alipofika mbele ya wajane waliokuwa wanalia na wameshuka moyo sana pamoja na kukata tamaa kabisa aliwatoa wote nje na kisha akasema **TABITHA "GET UP"** (Simama/ amka) na alipoinuka watu wengi wakaokoka. ***Mdo 9:36-42*** (Imani za wajane hawa zikajengwa upya na shuhuda zao kuhusu Yesu zikaongezeka.

**Note: Ilibidi Mungu ashughulike na Ibrahimu na Sara mkewe sana juu ya eneo hili la kufahamu kwamba kuna kuzaa tena hata kama umri wao umeenda na desturi za kuzaa zimekoma. *Mwanz. 17:15-19, 18:1-14, Mwanz 21:1-7***

- Ni kawaida kabisa ya Ibilisi kuwafanyia wateule/ watoto wa Mungu mambo ambayo yanawafikisha mahali pa kukata tamaa kabisa na kufikia hali ya kutoamini kwamba Mungu bado anaweza kuwaponya au kuwabariki n.k **na sisi Watumishi wa Mungu tunaposema kwao kuwa hilo bado linawezekana kwa Mungu aliye hai, tunaonekana kama tunawadanganya. *2Wafal 4:11-16!!* (Haya maneno ya huyu mwanamke ni sawa na maneno yale yale aliyoyasema Ibrahimu na Sara Mkewe wakati walipoambiwa kwamba watapata mtoto!!**

3. Mbele za Mungu, usiangalie tatizo/ jaribu lako limechukua muda gani na kamwe usiruhusu hali ya kukata tamaa itawale ufahamu wako,wewe pata ufahamu leo kama Ayubu kwamba **KUNA KUINUKA TENA!! *1Samwl 2:7-8, Zab. 113:7-8.*** Bwana anatenda kwetu jinsi atakavyo na kwa wakati wake; anatuinua sisi ambao tulidharauliwa na kubezwa kila kona hata na ndugu zetu. ***Mwanz 41:14-45.***

4. Tumwone Bwana anavyosema yeye mwenyewe na mtu wake ambaye anapitia katika majaribu pamoja na maumivu na mateso makubwa katika ulimwengu huu**. *Isay 54:1-17.***

a. ***Isaya 54:1-3.*** (**Imba wewe uliye tasa.** Yalikuwa ni maneno ya kuwatia moyo sana Wayahudi waliokuwa uhamishoni wakiteswa ili wafahamu kwamba kuna wakati wa Baraka tele na furaha tele vinakuja mbele yao, na watakuwa wengi kuliko hata wale waliochukuliwa kwenda uhamishoni!! Kauli hii iliwafanya wasitishe hali yao ya kulalamika pamoja na kumnung'unikia Mungu daima

b. ***Isaya 54:4-8***. (**Usiogope)** Mungu alikuwa anawataka wafahamu kwamba " **AIBU WALIYO NAYO HAITADUMU JUU YAO MILELE"** Mungu atatoa njia kwa ajili ya wokovu wao (**Aibu ya ujana wako (Mst4)** Hapa Mungu alikuwa anamaanisha kwamba mashutumu na dhihaka zote walizofanyiwa katika kipindi chote cha utumwa kule Babeli, vyote vitabaki historia watatoka kwa jeuri na kwa kicheko. ***Kut 14:8 (Kut 10:25-26***) Kama ilivyokuwa wakati wanatoka mikononi mwa Farao huko Misri.

c. ***Isaya 54:9-10*** (**Sitakuonea hasira wala kukukemea).** Unabii huu ulikuwa unamaanisha kwanza kabisa kile kipindi cha utawala wa Yesu Kristo pamoja na watu wake cha miaka **1000** ***(Ufun 20-22)*** lakini zaidi alikuwa anamaanisha kwa Taifa lake kwamba hataendelea kunyamaza wakati Taifa lake linaendelea kuonewa na kuteswa na adui!! (**Wakati wa Bwana kuangalia tu wakati shetani anatunyanyasa umekwisha**").

d. ***Isaya 54:11-17.*** (**Uliyeteswa, Uliyerushwa na tufani na usiyetulizwa!!** Haya yalikuwa ni maneno mazito sana ya faraja kwa wote ambao wanapitia katika hali ya mateso makali yanayosababishwa na adui. **Bwana Yesu hatavumilia wala hataendelea kuangalia tu wakati shetani anatunyanyasa ngo!!**

- Nami nataka wateule mfahamu kwa kina sana ninachosema siku ya leo kwamba "**Pale ambapo mwana wa Mungu unajikuta unaelemewa sana na majaribu mazito ambayo yanapelekea hata imani yako kuanza kutikiswa na tufani nyingi katika maisha haya; leo nataka ukumbuke kwamba" kuna kuinuka tena!! Nyakati unazopitia ndizo zitakazosababisha Yesu Kristo asimame karibu na wewe na kukuhurumia na kisha kukukaribia kwa jinsi ya tofauti akiwa na baraka zako tele jambo ambalo litakufanya uinuke kiroho kabisa. Mark 4:35-41**
- Kila mmoja wetu anao urithi kutoka kwa Bwana wetu Yesu Kristo na kama yeye alivyoinuka tena kutoka kwa wafu; nasi siyo tu kwamba tutafufuliwa siku ile ya Parapanda ya mwisho, bali kuna kuinuka tena katika mambo yetu ya maisha haya na kuwafanya wengi watushangae na kumwamini Yesu wetu. **Amina**

***Na***
***Askofu Dr. L. M. Mwizarubi***
***10/07/2022***